JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BENKI KUU YA TANZANIA

20 Novemba 2026

TAARIFA KWA UMMA

USIMAMIZI WA WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA WASIOPOKEA AMANA (DARAJA LA PILI) ZANZIBAR

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inautaarifu umma kuwa imepewa jukumu la kusimamia na kufuatilia watoa huduma ndogo za fedha Zanzibar kwa mujibu wa vifungu vya 15 na 16 vya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar Na. 9 ya Mwaka 2023. Sheria hiyo iliyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar (BLW), ilianza rasmi kutumika mwaka 2025 kufuatia kutangazwa na Waziri wa Fedha Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar ya Mwaka 2019.

Ili kutekeleza Sheria hiyo kwa ufanisi, Wizara ya Fedha Zanzibar kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Fedha iliandaa Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (Wasiopokea Amana - Daraja la Pili) ya Mwaka 2025. Kanuni hizi zimeweka utaratibu na vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa katika utoaji wa leseni, mitaji pamoja na masuala ya utawala wa taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha.

Hivyo, watoa huduma ndogo za fedha (wasiopokea amana - Daraja la Pili) wanaotoa au wanaotarajia kutoa huduma hizo Zanzibar wanatakiwa kuwasilisha maombi ya leseni Benki Kuu ya Tanzania - Zanzibar kuanzia tarehe ya tangazo hili. Kwa wale ambao wanaendelea kutoa huduma, mwisho wa kuwasilisha maombi hayo ni tarehe 31 Disemba, 2026.

Umma unakumbushwa kuwa, ni kosa kisheria kwa mtu au taasisi yoyote kufanya biashara ya kutoa huduma ndogo za fedha bila kuwa na leseni ya BoT au Mamlaka iliyokasimiwa, kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar Namba 9 ya Mwaka 2023.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania, au wasilisha barua pepe kwa Hamad.Hamad@bot.go.tz; Dickson.Gama@bot.go.tz; na Mary.Ngassa@bot.go.tz au piga simu namba +255 26 2963182 au +255 22 2232541.

Emmanuel M. Tutuba
GAVANA

16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P. 2303, 40184 Dodoma - Tanzania,
Barua Pepe: governoroffice@bot.go.tz, Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2541/2501